

KEJELI NA FASIHI YA KISWAHILI - TANZANIA

STEVEN ELISAMIA MRIKARIA

Irony is a widely used device which plays a large role not only in conversation, but also has impacts on our daily thoughts. In literature, the device of irony has been used in the past and it is still being used by writers today so that readers can think deeply on the presented topic and understand the message and the intended concept. Wamitila (2008: 409) finds that irony is among the many devices which facilitate our conversations, mostly with its capability of indirectly revealing our hidden feelings, views and perspectives. According to Mbatiah (2001: 27) irony is a concept used in speech which can cause a painful realization.

This article discusses the methodologies and different strategies applied in the use of irony within Kiswahili literature. The main argument within the article is that irony can cause the reader to indirectly recognize a deeper meaning within the text. The basic assertion in this article is to highlight how irony has played a large role within Kiswahili literature before independence, after independence, within the Arusha Declaration, and up until this time of globalization.

Kejeli ni mbinu pana, ambayo huchukua nafasi kubwa na kutoa mchango wake si katika mazungumzo tu bali pia katika utoaji wa mawazo yetu ya kila siku. Katika fasihi, mbinu ya kejeli imetumiwa na inaendelea kutumiwa na waandishi ili kuiwezesha hadhira/wasomaji wafikirie kwa undani suala linaloongelewa ili waweze kupata ujumbe uliokusudiwa kufikishwa kwao. Wamitila (2008: 409) anasema kuwa, kejeli ni mojawapo ya mbinu zinazotawala maongezi yetu hasa kutokana na uwezo wake wa kuficha hisia, maoni na mitazamo yetu sahihi. Kwa maoni ya Mbatiah (2001: 27), kejeli ni maneno yanayotumiwa katika matamshi kama hayo huwa ni ya kuchoma, kukata na kutia uchungu.

Makala haya yanajadili kwa kina njia na mbinu mbalimbali zilizotumika katika kutumia kejeli katika fasihi ya Kiswahili. Mbinu inayoongoza makala ni ile inayoitambua kejeli katika hali ambapo kuna kinyume na Fulani katika usemi, hali au tukio. Suala la msingi katika makala haya ni kuonyesha jinsi mbinu ya kejeli ilivyooneshwa katika Kiswahili kuanzia kabla ya uhuru, baada ya uhuru, azimio la Arusha hadi wakati huu wa utandawazi kumeisaidia kwa kiasi gani jamii ya Kitanzania.

1. Utangulizi

Katika fasihi ya Kiswahili, zipo kazi nyingi ambazo zimejikita katika dhana ya kejeli. Kejeli katika kazi hizo imetumika kuielezea historia ya Tanzania kuanzia kabla ya uhuru, baada ya uhuru, baada ya Azimio la Arusha na hata hivi sasa. Katika fasihi ya Kiswahili, kazi hizo ni nyingi kiasi kwamba ni vigumu kuzipitia zote katika makala haya. Makala haya yatajaribu kuzichambua baadhi tu ya kazi na nadharia za magwiji wa fasihi ya Kiswahili. Kazi hizo zitakazochambuliwa ni: *Miradi Bubu ya Wazalendo* (Ruhumbika 1995); *Mashairi ya Cheka Cheka, Chungu Tamu na Raha Karaha* (Mvungi 1995, 1985 & 1978); *Nuru Mpya*, (Rutashobya 1980); *Pepo ya Mabwege* (Mwakyembe 1980); *Kaputula la Marx* (Kezilahabi 1999); *Karibu Ndani* (Kezilahabi 1988); *Fungate ya Uhuru* (Khatibu 1988); *Lina Ubani* (Muhando 1984); na *Kijiji Chetu* (Ngahyoma 1975).

KEJELI NA FASIHI YA KISWAHILI – TANZANIA

Kwa hakika kazi za waandishi hawa zinaelezea ki-maudhui mwelekeo wa Tanzania kabla ya uhuru, na mwenendo wa Tanzania huru hadi hivi sasa. Sababu zilizowafanya waandishi kama: Shaaban, Penina, Kezilahabi, na wengine kutumia fikra zao na kuandika kazi zinazoihusu jamii ni ufisadi, usaliti, unyanyasaji na dhuluma, viliyokuwa vimekithiri ndani na nje ya uongozi uliokuwepo madarakani. Viongozi hawa walianzisha matabaka ya watu, wakaendeleza rushwa, ufisadi na mambo mengine machafu katika jamii zetu. Tukiangalia kabla ya uhuru, Wakoloni waliwadhalilisha wananchi kwa kuwalaghai, waliwanyanyasa na kuwadhumu mali zao kwa hila na pengine kwa kutumianguvu. Baada ya uhuru viongozi waliochaguwa waligeuka kuwa Wazungu weusi na wakawa wakiiga matendo na mienendo waliyokuwa wakiifanya wakoloni. Aidha, hadi hivi sasa viongozi wetu wawapo madarakani hukengeuka na kuwa manyang'au, mafisadi, mafedhuli, wenye tamaa za madaraka na ujasiri wa kulikandamiza tabaka la wanyonge.

Kwa hali hiyo, waandishi hawa wameichora kejeli kwa kutumia fikra mbalimbali zikiwa ni pamoja na kuwatumia wahusika wa ushairi, riwaya na tamthilia. Taswira, ujumbe na hata mpangilio wa maudhui ya kazi za waandishi wa fasihi vimelenga katika kuwasema watu hawa waliobeba dhamana kubwa kwa jamii zao. Kwa kuzingatia maudhui ya kazi zao, waandishi hawa wametuonesha madhara ya uongozi mbaya, madhara ya rushwa, ubadhirifu wa mali ya umma, n.k. Na kuweka mikakati ya namna ya kuudhibiti uongozi kama huo kwa njia ya kejeli.

Makala haya yatajikita katika kuelezea jinsi baadhi ya waandishi wa kazi za fasihi waliyokuwa mahiri katika kutumia mbinu ya kejeli wakati wa kuandika kazi zao za wakati huo. Makala yataangalia pia jinsi kejeli hizo zilivyoibua maudhui ya dhana nzima.

2. Kejeli na fasihi

Kejeli hutumia nafasi kubwa katika jamii si katika mazungumzo ya kila siku tu, bali pia namna wanajamii wanavyoyatoa mawazo yao katika uwanja wa mawasiliano. Kwa maneno mengine, tunaweza kusema kwamba, ni mojawapo ya mbinu zinazotawala mazungumzo ya wanajamii ya kila siku. Kejeli hujengwa katika msingi wa kuwepo na msigano au mgongano wa namna fulani kati ya hali ya maisha na matarajio ya baadae ya wanaohusika.

Katika fasihi mbinu ya kejeli hupatikana katika mawanda mapana na ya aina mbalimbali. Kuna kejeli ambayo zinapatikana zaidi katika utanzu wa tamthilia kuliko katika riwaya (ingawa hii haimaanishi kuwa haijitokezi kabisa katika riwaya). Aidha zipo kejeli zinazojengwa kwa matumizi ya maneno yenye kutegemea mgongano wa hali au jaala ambayo tutaangalia baadaye.

Kundi la kwanza na ambalo ni la asilia katika fasihi, lenye kubeba mzigo mkubwa wa kejeli ni fasihi simulizi. Kundi hili lina tanzu, zilizogawanywa katika makundi makuu manne: hadithi, ushairi, semi na sanaa za maonyesho. Hata hivyo, kila utanzu umegawanywa katika

STEVEN E. MRIKARIA

vikundi vidogovidogo vijulikanavyo kama vipera. Vipera tutakavyoviangalia zaidi katika makala haya ni vile vya semi na vya sanaa za maonyesho.

Vipera vya semi katika fasihi simulizi ni methali, vitendawili, nahau, misemo na misimu. Wamitila (2008: 410) anasema kuwa

kejeli ya kiusemi inaelezwa kama ni kejeli ya msingi sana na hutokea pale ambapo pana mkinzano fulani baina ya kile kinachosemwa na uhalisia wenyewe.

Anasema kwamba,

uelewaji wa kejeli ya kiusemi huhitaji msemaji na msikilizaji au hadhira kuwa na hisia au mwelekeo fulani kuhusu mada inayozungumziwa.

Maneno ya Wamitila yana ukweli ndani yake kwa sababu si rahisi kwa jamii yenye utamaduni usiofanana na jamii nyingine kuelewa barabara semi za kejeli vizuri sawasawa na jamii husika. Vipera vingine kama methali, vitendawili, nahau na vinginevyo hutumia sanaa mahsusi kuipa lugha uhai (Mtesigwa 1989), zenye kutoa mafunzo mazito yanayotokana na uzoefu wa jamii (Mulokozi 1989), misemo itumiwayo hueleza kitu kwa njia ya picha na kwa ufupi ili kutoa adili au onyo (Balisidya 1982). Hapa pia tunaweza kukutana na kejeli ya dhihaka ambayo msingi wake mkuu unajengwa juu ya kejeli ya kiusemi. Kejeli hii hujitokeza pale maneno msemaji anayoyasema hayamaanishi tu kinyume chake bali yanakusudiwa kumfanya msemwaji akereke, audhike, akosoleke au arekebike yanapozungumzwa. Kwa mfano kauli kama: *huku kweli ndiko kupendana kwetu*. Hapa msemaji anatumia kejeli, hamaanishi kupendana kwa kweli bali *huku kweli ndiko* na *kupendana kwetu* kunaufanya uwe kejeli na dhihaka ndani mwa usemi huo.

Vipera vya sanaa za maonyesho havitegemei semi au maneno yasemwayo tu bali hutegemea pia maneno yaandikwayo pamoja na sifa nyingine zinazohusiana kuona zisizokuwa za kimaneno au semi. Hapa tunaweza kukutana na majigambo, matambiko, ngoma, miviga (sherehe), kejeli (kinaya) na mengine mengi ambayo hatuhitaji kuyachanganua.

Kundi jingine ambalo linapatikana katika mawanda ya fasihi, na ambalo ndilo msingi wetu mkuu ni lile linaloweza hata likahifadhiwa katika maandishi. Tangu za kundi hili ni riwaya, tamthiliya, hadithi, novela, tawasifu, hadithi fupi na ushairi. Katika kuliangalia kundi hili, tunaona kwamba, kuna kejeli ambazo zinapatikana sana katika kundi moja kuliko kundi jingine. Mathalani, katika utanzu wa tamthiliya, kejeli inapatikana na kutumika zaidi kuliko katika tanzu za riwaya, hadithi, novela, tawasifu, hadithi fupi na ushairi. Hapa hatumaanishi kwamba kejeli hazitumiki katika tanzu hizo, bali hutumika kwa kiwango kidogo sana.

Wamitila (2008: 409) anatumia kwamba:

zipo kejeli ambazo hujengwa kwa matumizi ya maneno (nyenzo) tofauti na nyingine ambayo hutegemea mgongano wa hali au jaala.

Hapa tunakiri kwamba, pamoja na kuwepo kwa matatizo na ugumu mkubwa katika kuainisha na kugawa makundi mbalimbali ya kejeli katika fasihi, makala yatatazama kejeli kwa kutumia tanzu chache tu za fasihi kama msingi wa kuainisha na kuonyesha uwepo wake.

KEJELI NA FASIHI YA KISWAHILI – TANZANIA

Kama tulivyokwisha kuona mizizi ya kejeli inaanzia katika semi na kumalizikia katika sanaa za maonyesho. Kejeli ni usemi au maneno yanayoumiza yasemwapo, yazungumzwapo na hata yaandikwapo. Hapa tunamaanisha kuwa, kejeli yaweza kuwa aidha maneno au semi inayokusudiwa kungusa mtu kwa njia ya waziwazi ambapo aghalabu ni kwa nia ya kufichua ubaya au udhaifu fulani alionao mhusika fulani, ama maneno au semi ambapo kuna kinyume fulani katika usemi, hali au tukio fulani. Kwa mfano, mtu fulani amepatwa na janga fulani, marafiki zake huweza kufurahishwa sana na janga hile lililompata moyoni. Ila kwa upande mwingine, usoni marafiki hawa hawaoneshi kufurahishwa kwao na hayo mabaya yaliyompata, bali wanajionesha kuwa wako pamoja naye katika huzuni yake hiyo. Hapa tunaona kuwa, ile hali ya kujionesha kuwa marafiki zake wapo pamoja naye katika huzuni, inageuka kuwa furaha kwa yale yaliyompata.

Kwa upande mwingine tunaweza kuona kejeli nyingine kwa mfano mhusika fulani anamcheka mhusika mwingine aliyepatwa na matatizo fulani kama msiba fulani ilhali msiba kama huohuo unamtokea na yeye (na labda yeye mwenyewe hajui). Hii ni kejeli ambapo utokeaji wa jambo au mambo unakwenda kinyume na hali au matarajio ya msomaji au mhusika anayepatikana katika kazi fulani.

Kwa kupitia mifano ya kejeli tuliyoona hapo juu, tunaweza kuhitimisha kwamba, mwandishi huweza kutumia kejeli kufikisha ujumbe wake kwa hadhira iliyokusudiwa bila kuiathiri hadhira yenyewe. Maudhui na ujumbe wa mwandishi uliobebwa na kejeli kwa hadhira yanaweza kutimizwa na kuirekebisha jamii ili iende sambamba na maadili yaliyokusudiwa.

3. Kejeli na fasihi ya Kiswahili

Kamusi ya Wales (2001: 224) inasema kuwa:

Kejeli hutokea pale ambapo maneno yanayotumiwa yanaelekea kukinzana na maana inayohitajika katika muktadha maalumu na inayokusudiwa na mwandishi, msemaji au mtumiaji. (tafsiri ya mwandishi)

Hapa tunamaanisha kuwa kejeli huangalia mbinu ya ulaghai, kinyume cha mambo, udanganyifu au masimulizi yasiyo na ukweli ndani yake katika kumzungumzia, kumkebehi au kumteta mtu fulani. Mbinu ya kejeli huonyesha vituko na mbwembwe nyingi zinazopelekea kufurahisha, kuteta, kufunza na kuonya kiasi kwamba si rahisi kuvitambua, kuvikubali au kuvikataa ndani ya jamii. Mara nyingi mbinu hii huwepo mahususi kwa lengo la kuteta au kuweka hadharani yale yaliyo kinyume na matakwa ya jamii. Aghalabu kama semi au maneno haya yatakuwa yamekusudiwa kumsema au kumwambia mtu fulani huishia kumkejeli mtu huyo si kwa uwazi. Short (1980: 277) anafafanua mbinu ya kejeli kwamba ni

ushirikiano wa siri kati ya mwandishi au msemaji na msomaji, msikilizaji au hadhira. (tafsiri ya mwandishi)

Hii inatutia hamasa pengine kuangalia matumizi ya semi katika maeneo mbalimbali ya tanzu za fasihi. Kwa mfano, iwapo wewe ni mgeni wa lugha na ukaamua kutembelea tanzu

STEVEN E. MRIKARIA

mbalimbali za fasihi na kuvinjari katika vipera kadhaa vya semi na kukutana na watu waki-
semezana kwa sauti:

Mke ni nguo, Mgomba kupaliliwa!

Vizee vyangu viwili kutwa vinatwanga.

Hapa kunatokea utata wa aina fulani na ambapo wengi huwa wanajiuliza kuwa semi hizi zina-
maanisha nini?

Kwa hakika ukiziangalia semi hizi, huwezi kuelewa linalosemwa hadi uzame ndani zaidi
katika kuchambua maudhui yake. Hapa semi inamaanisha kuwa ni fungu la maneno yanayo-
tumiwa katika jamii yakiwa na maana iliyofichika, yenye kutoa maana fulani. Mara nyingi
semi hutumika katika lugha ya uficho ya picha, tamathali na ishara, hivyo kumfikirisha sana
mtu au jamii katika kupata maana iliyokusudiwa. Kwa upande mwingine, haya ni mafumbo
yenye kubeba maudhui yenye maana zinazofuatana na ibara mbalimbali. Usemi *Mke ni nguo,*
Mgomba kupaliliwa unaweza kunyambuliwa kuwa: *mgomba* na *nguo* vinasimama upande wa
mwanamke, vikimamanisha kuwa ili mke aweze kupendeza ni lazima atunzwe kwa manufaa
ya mwanaume. Hii ni methali yenye kutumia picha.

Usemi wa pili *Vizee vyangu viwili kutwa vinatwanga* ni kitendawili, chenye maana iliyo-
fichika. Mwenye kujua maudhui ya kitendawili hiki atajibu kwamba jibu lake ni *kope za*
macho.

Hapa tunaweza kusema kuwa, kama hutakuwa na mtu wa kukueleweshwa maana iliyo-
fichika ndani ya maneno haya, utadhania kuwa watu hawa wanatukanana, wanakaripiana au
wanagombana. Hali hii ndiyo unayoweza kukutana nayo wakati unapozungumza, unaposoma
au unaposikiliza masuala yenye kejeli ndani yake.

Kejeli katika fasihi ya aina hii ni mbinu ya kifani ambayo waandishi wanaitumia ili kum-
fanya msomaji afikirie kwa dhati na kwa kina ili aweze kupata ujumbe uliokusudiwa kwa
jamii yake. Waandishi hawa wa fasihi ya Kiswahili wameitumia mbinu hii ili kumulika, ku-
chunguza na kuonyesha wazi mambo yaliyokithiri katika jamii. Mambo hayo yaliyopo
kwenye jamii ni pamoja na uongozi mbaya; rushwa; ubadhirifu, unyang'anyi, wizi wa mali ya
umma, ubepari, ubwanyenye, na maovu mengine mengi yanayofanana na hayo ambayo yana-
rudisha nyuma maendeleo ya jamii.

3.1. Kejeli na fasihi kabla ya uhuru

Kabla ya Ukoloni waandishi wa kazi za fasihi ya Kiswahili walitumia mbinu ya kejeli katika
kuwasema wavivu na wale wote waliokuwa wakienda kinyume na maadili ya jamii. Tanzu za
fasihi simulizi kama vile nyimbo, hadithi, ngonjera, methali na misemo zilitumika katika kui-
kosoa jamii hiyo. Kejeli ilitumika kama mbinu ya kusemana, kukosoana, kuonyana na hata
kurekebishana katika jamii. Aidha ni katika mbinu ya kejeli kazi ya fasihi ilitumika kufi-
kirisha hadhira na maudhui kwa hadhira yake yaliyomo katika jamii ili waweze kujitambua na
kujikosoa bila kutajwa.

KEJELI NA FASIHI YA KISWAHILI – TANZANIA

Kwa mfano, upo msemu wa Kiswahili usemao *Anapenda mteremko* au *anapenda dezo* hutumika ukimaanisha kuwa mhusika anapenda vitu vya bure. Msemu huu ni kejeli kwa watu ambao hawataki kujishughulisha na kazi ngumu au za sulubu, hivyo hupenda vya bure bila kufanya kazi.

Halikadhalika kuna misemo kama vile kumwita mtu ambaye hapendi kushirikiana na wenzake katika kazi *Bwana mkubwa*. Huku ni kumkejeli kwamba yeye ni mkubwa hivyo hawezi kushiriki na wenzake katika kazi. Lakini kwa upande mwingine ukiangalia hali ya mtu huyo anayeitwa *Bwana mkubwa* huwezi kuona uhusiano kati ya mtu huyu na jina alilopewa, ila kinachobainishwa hapa ni matendo ya mtu huyu.

Waandishi wengi walitumia mbinu mbalimbali za kifani katika kufikisha ujumbe wao kwa jamii. Kwa mfano, wakati wa Ukoloni fasihi ya Kiswahili ilitumika katika kusawiri hali halisi ya maisha ya wakati huo. Waandishi hawa waligeuza mbinu zao za uandishi na kutumia mbinu ya kejeli katika kuonesha jinsi jamii ilivyokuwa ikinyanyasika, ikionewa, na iki-tawaliwa kinyama, hali ambayo ikiwakosesha amani katika maisha yao ya kila siku.

Katika kazi ya Ruhumbika (1995) ingawa iliandikwa katika kipindi cha baada ya ukoloni, tunamwona akitumia kejeli katika kuonesha matabaka makuu yaliyokuwepo katika kipindi cha Ukoloni. Kwa mfano, mwandishi ametumia jina la mhusika *Tumbotumbo* kuwakilisha tabaka la mabwenyenyeye, watawala na wenye mali nyingi. Kwa kutumia neno *Tumbotumbo*, mwandishi alifanikiwa sana kuwasema wazungu kuwa walikuwa wakilionea tabaka la chini kwa manufaa yao. Kwa lugha ya kawaida *Tumbotumbo* ni mtu mwenye kupenda sana kula na asiyesumbukia suala jingine isipokuwa tumbo lake tu. Katika kazi hii anatuonesha kuwa tabaka la Wakoloni lilikuwa likilidhalilisha, likilitumikisha, likilinyonya na likilikandamiza tabaka la chini yaani lile la watawaliwa. Mbinu hii imemwezesha mwandishi kufanikisha suala zima la kifani katika kuonesha kuwa, Wakoloni walikuwa na dhima ya kujinufaisha wenyewe (matumbo yao) na jamii zao na si kujishughulisha na maisha ya watawaliwa au walalahoi.

Mbinu nyingine zilizotumiwa na waandishi hawa ni kwanza, ujenzi wa mandhari ya hisia kama inavyoonekana katika kazi hizi mbili za Kandoro (1971). Katika kazi hii tunaona mwandishi ametumia taswira ya mafumbo mazito na kejeli ambazo haikuwa rahisi kwa Wakoloni kuzigundua kwa urahisi. Kwa mfano, ametumia msemu *Siafu wamekazana* (Kandoro 1971: 138) akiwakejeli Wakoloni ili wasifahamu kuwa Watanzania wamekwisha-amshwa na kuanza harakati za kudai uhuru.

STEVEN E. MRIKARIA

Nyoka amegutuka, ndani ya shimo kutuna,
Tena amekasirika. hasira zenye kununa,
Nyoka anababaika, shimoni kwa kujikuna.
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.
Shimoni ataondoka, hilo nataja kwa jina,
Nyoka anajua fika, siafu wakiungana,
Nguvu zinaongezeka, shimoni watagombana,
Siafu wameungana, nyoka amekasirika.
Siafu zikijishika, mshiko kushikamana,
Kwamba zinampeleka, sultani wao bwana,
Shimoni zinapojika, nyoka fa kufanya hana.
Siafu wameungana, nyoka amekasirika.
Siafu wanapofika, na nyoka wakikutana.
Nyoka hawezi kufoka, huwa ametulizana,
Ndipo nyoka hundoka, na wana wakilizana.

Hapa siafu kwa upande mmoja ni neno linawaunganisha wanajamii kwa pamoja ili waweze kuungana kama siafu kumng'oa Mkoloni. Na kwa upande mwingine neno hili lina maana ya kuunda jeshi na kuliunganisha ili liwe na nguvu ya kumshambulia Mkoloni.

Kazi nyingine zilizotumika katika mapambano dhidi ya ukandamizwaji wa jamii na Wazungu kwa kuwakejeli ni kama vile misemo na methali mbalimbali. Kwa mfano, katika kitendawili hiki *Wazungu wawili wanateremka mlima* jibu likiwa ni *Makamasi*. Kwa kuzingatia maana ya kitendawili hiki, kwa upande mmoja tunaona jinsi mzungu alivyokuwa ana-kejeliwa kuwa ataondolewa kama kamasi.

Katika kupambana na Wakoloni wa wakati ule, ilifanyika kazi ngumu sana, ndio sababu waandishi wakaandika mengi katika kuwakejeli Wazungu. Hapa tunamaanisha kwamba, wapo baadhi yetu miongoni mwa wanajamii waliokuwa wakifurahia kuwepo kwa Wazungu hao kwa kuyaiga matendo waliyokuwa wakiyafanya. Watu hawa walikejeliwa kupitia kazi mbalimbali zilizoandikwa na waandishi wa fasihi. Kazi ambazo ziliwakejeli watu hawa walioacha mila na desturi zao na kufuata utamaduni wa kigeni zilikuwa nyingi. Miongoni mwa kazi hizi ni nyimbo mbalimbali zilizoimbwa katika harakati za kudai uhuru kutoka kwa Wakoloni.

3.2. Kejeli na fasihi baada ya uhuru

Katika kipindi hiki, wanajamii walikuwa na matumaini ya kuwa na maisha bora ya kujitawala wenyewe na kuacha kutawaliwa na wageni. Mambo yaligeuka na kuwa kinyume na yale waliyotarajia. Viongozi wengi walioingia madarakani, waliiga yale yote waliyokuwa wakiyafanya Wakoloni. Matokeo yake yakawa kinyume kabisa na matarajio ya wanajamii hawa. Kuka-tokea kuwa na uongozi mbovu, uliokuwa na uroho wa kutafuta mali kwa manufaa yao

KEJELI NA FASIHI YA KISWAHILI – TANZANIA

wenyewe. Katika uongozi pakaibuka ubadhirifu, wizi na ufujaji wa mali ya umma. Rushwa, unyang'anyi, unyanyasaji, ubeberu, ufisadi vilikithiri kwa baadhi ya viongozi.

Fasihi ya Kiswahili haikulifumbia macho suala hili. Ziliandikwa kazi nyingi zilizokuwa zikiwasema, zikiwakosoa na zikiwakejeli vibaraka na wasaliti hawa. Kwa mfano, katika riwaya ya Ruhumbika (1995) *Miradi Bubu ya Wazalendo* amewakosoa viongozi katika kuonesha hali halisi ya maisha katika kipindi hicho. Ameweka wazi rushwa na usaliti uliofanywa na viongozi waliojilimbikizia mali. Hapa anatuonesha matabaka, uchu wa madaraka, usaliti na uhujumu wa uchumi uliokithiri katika jamii. Kwa mfano, katika ukurasa wa themanini na moja, anasema:

Kila mtu mwenye fursa kwenye ofisi za serikali, kwenye mashirika ya umma, ugawaji na usagishaji, kwenye maduka ya kaya, akakazana kuhakikisha hiyo kazi yake au madaraka yanamtajirisha iwezekanavyo, matokeo yake wizi, magendo na ulanguzi vikatia fora na ikawa kila kitu hakinunuliki tena...

Miongoni mwa kazi zilizokuwa na kejeli ni nyimbo mbalimbali zilizoitumbwa katika harakati za kudai uhuru kutoka kwa Wakoloni. Katika nyimbo hizi dhana ya kejeli ilitumika ili kufanya jamii ifikiri kwa kina ubaya wa matendo yaliyofanywa na Wakoloni dhidi ya jamii. Kwa mfano, katika wimbo *Twamtaka Mtemvu* tuliokuwa tukiuiimba tulipokuwa katika *Jeshi la Kujenga Taifa* (JKT):

Twamtaka Mtemvu, tamlam mmh
Tumuone eh, tamlam mh
Twamtaka Mtemvu ee Tumuoee ee
Mtu kama huyu, tamlam mmh
Msalitii, tamlam mmh
Mtu kama huyu ee! Msalitii ee!

Historia inanatujaza kwamba, Mtemvu alikuwa ni mpinzani mkuu wa chama cha TANU wakati chama hiki kilipokuwa kinadai uhuru kutoka kwa Wakoloni. Ili kuweza kumrejsha kwenye chama cha TANU kwa amani ilibidi dhana ya kejeli itumike. Kutokana na nyimbo mbalimbali za kumkejeli aliweza kurekebishika na kujiunga na chama cha TANU. Hapa ndipo fasihi ya Kiswahili ilipoingia katika hatua nyingine mpya.

Wapo waandishi wengine walioitumia mbinu ya kejeli kama njia mojawapo ya kuonesha machungu yaliyokuwapo katika jamii huru. Mwandishi aliyefanikiwa kutumia kejeli ya namna hii katika kuonesha machungu ya udanganyifu wa kimaendeleo, wizi, dhuluma, umaskini na uongozi mbaya unaofanywa na viongozi waliokuweco madarakani ni Mvungi (1985). Katika mashairi ya *Chungu Tamu* anakejeli suala zima na umaskini katika jamii na chanzo chake. Katika shairi lake *Chanzo ni Wenye Kauli* anasema katika ukurasa wa ishirini na nane:

(...) Ni watu katili, Kwa uroho na akili
Wakajitwalia mali, Kwa idhini na vibali
Chanzo ni wenye kauli, Tumakinike na hali (...)

STEVEN E. MRIKARIA

Mwandishi ametumia kichwa cha shairi hili kuonesha chanzo cha umaskini na hali ngumu ya maisha katika jamii. Hapa mwandishi kwa kutumia kejeli anaweka wazi kwamba viongozi wanaoitawala jamii yetu ndio chanzo cha hali ngumu ya maisha na umaskini kwa wananchi walio katika tabaka la chini. Hapa anamaanisha viongozi ndio wenye kuonja *Tamu* wakati wananchi wakila *Chungu*.

Ni katika kipindi hiki, ndipo wanajamii walipotambua kuwa maisha yao si bora kama walivyokuwa wametarajia. Waligundua kwamba, viongozi wengi walioingia madarakani, walikuwa wakifanya zaidi ya yale waliyokuwa wakifanya Wakoloni. Kazi ya Ruhumbika (1995) *Miradi Bubub ya Wazalendo*, pamoja na kwamba, ilikuwa ikisawiri miaka hamsini ya historia ya Tanzania, ilionyesha kejeli ilivyokuwa ikitumika. Katika kazi hiyo, tunaoneshwa jinsi viongozi walivyokuwa wakiwanyanya wanajamii waliokuwa wamewachagua kwa kura zao. Kwa mtazamo wa nje tu, jina la riwaya *Miradi Bubub ya Wazalendo* linamkejeli mzalendo na jamii nzima ya kuwa hawana jipya la kuweza kufanya kwa kuwa yote wanayo-yawaza hayatekelezeki. Mwandishi anawataka wanajamii kujitokeza kuibua mawazo na kuhimiza mapambano ili kuutetea ukombozi utakaowaletea uhuru wa kujenga jamii mpya.

Kutokana na hayo, fasihi nayo haikulala. Ilitumia mbinu mbalimbali katika kuweka wazi mambo yaliyohitaji kutekelezwa kwa wakati huo ili kuhakikisha kwamba viongozi hawapati amani. Waandishi wengi walitumia tena kejeli katika kufichua uchafu huo ambao ulikuwa kero kwao. Mmoja wa waandishi hao ni Khatib¹ na diwani yake ya *Fungate ya Uhuru* (1988). Katika diwani hii, mwandishi ametumia mbinu za kisanaa kuyakejeli maisha ya viongozi hao wa baada ya uhuru. Kwanza kabisa neno *Fungate* ni kejeli kwa viongozi ambao baada ya uhuru waliishi maisha ya raha mustarehe wakifaidi matunda ya uhuru bila kujali wananchi wanaowaongoza. Khatibu (1988) ametumia *Fungate ya Uhuru* kama jina la kitabu na kama kichwa kimojawapo cha mashairi yake katika kuonyesha uhuru unaosemekana umepatikana katika jamii yetu. Kwa mfano, katika shairi la *Fungate* ukurasa wa kwanza:

Fungate ya uhuru, Bado inaendelea
Harusi wana uhuru, Wazuri wanavutiya
Wengi inawadhuru, Na tena wanaumiya ...

Hapa mwandishi anaonyesha umahiri wake wa kutumia kejeli katika kuwaumbua viongozi waliopewa dhamana ya kuiongoza jamii. Tunaona jinsi alivyoweza kutumia kejeli akafaninisha *Uhuru* na harusi ambayo wapo wachache wanaoifaidi na kuifurahia *Fungate* hiyo ambao ni viongozi. Akaonesha pia walio wengi na ambao hawaifurahii *Fungate* hiyo ambao ni wananchi.

Pia tunapoangalia shairi la Khatib la *Mjamzito*, mwandishi anaiweka wazi kero iliyopo katika jamii. Katika shairi hili anatumia kejeli ya mama mjamzito asiyeweza kuondokana na mzigo wake wa mimba hadi hapo siku ya kujifungua itakapofika. Hii ina maana kwamba

¹ Mhe. Muhammed Seif Khatib ni Mbunge na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano Katika Serikali ya Muungano wa Tanzania.

KEJELI NA FASIHI YA KISWAHILI – TANZANIA

anawahamasisha wanajamii wasibweteke, bali wahamaki juu ya kero hiyo na kujibidiisha ili kuleta mapinduzi ya kweli. Hapa anaiona jamii kama imefungwa na haiwezi kujifungua.

Analinganisha mateso na mahangaiko aliyonayo mama mjamzito na jamii tunayoishi iliyojaa kero na ghadhabu ya viongozi wanaojali matumbo yao na kusahau wananchi waliowachagua. Mfano, shairi *Mjamzito*:

Mjamzito, Amelazwa “thieta”!
Lazima kupasuliwa,
Chake kitoto, Tumboni kinatweta
Hawezi kujifungu

Kwa upande mwingine, katika tamthilia ya Rutashobya (1980) *Nuru Mpya*, tunaona ametumia kejeli kuonesha kuwa, viongozi wetu badala ya kutumia muda wao kwa kutatua matatizo ya umma, wanatumia muda wao kutafuta njia za kujitajirisha wenyewe. Katika tamthilia hii anatuonesha jinsi vijana ambao ndio *nuru mpya* wanavyoamua kujitoa muhanga ili kukomesha unyonyaji, ukosekanaji wa haki za wananchi na ukosekanaji wa maendeleo katika jamii.

Mwandishi ametumia majina ya wahusika wake kama kejeli kwa matendo yafanywayo na viongozi katika jamii. Kwa mfano, mwandishi ametumia majina kama *shoka, rungu, nuru, mapanga*, n.k. ili kuonesha kuwa uwezo wa wanajamii kupambana na dola iliyoko madarakani ni duni na hautawasaidia chochote. Aidha mwandishi anaiamsha jamii ili ifahamu kwamba, kama wakiungana na kujipanga pamoja kwa kutumia silaha (*shoka na rungu*) wanaweza kuung’oa uongozi mbaya waliouweka madarada na *nuru mpya* ambayo ni ukombozi wenye kuleta uongozi unaokubaliwa na wanajamii.

Rutashobya (1980) amefanikiwa kuifikishia jamii ujumbe kwa kuwakejeli viongozi kupitia maisha ya jamii ambayo inahitaji mapambano yenye kuleta ukombozi. Ukombozi anaouongelea mwandishi umeanza kujibainisha kwa viongozi wetu hivi sasa. Wananchi wa Tanzania wameiona *Nuru Mpya* pale walipooneshwa ubadhirifu wa fedha ya umma ndani ya Benki Kuu ya Tanzania.

Tamthiliya hii ya Rutashobya inaiamsha jamii ya Kitanzania hata leo kupigana na ufisadi hasa ule wa matumizi mabaya ya ofisi za serikali, fedha za umma na rasilimali za nchi. Rutashobya anawakejeli wale waliopitisha matumizi ya ujenzi wa nyumba mbili za Gavana wa Benki Kuu (BOT) na manaibu wake ya shilingi bilioni 2.5 kwa kutumia *Nuru Mpya* kuwa wangetiwa vitanzini ili kuwa fundisho kwa viongozi wengine.

Kama tukichunguza kwa makini, tamthiliya hii inaiamsha jamii kwa kupitia viongozi wachache wasafi kuleta na mageuzi na *nuru mpya* kwa watuhuma wa ufisadi katika akaunti ya Madeni ya Nje katika Benki Kuu ya Tanzania (BOT), ili jamii iweze kuwa na imani na viongozi hao. Mwandishi katika ukurasa wa nane, anasema kwamba: “viongozi ni ndugu zetu.” Hii inaonyesha tofauti iliopo kati ya viongozi watawala na watawaliwa katika hali halisi ya maisha. Hii inaonyesha kuwa ni kejeli moja kwa moja kwani kiongozi asiyewajali

STEVEN E. MRIKARIA

wananchi waliomchagua hawezi kuwa ndugu yao. Katika ukurasa wa tisa, mwandishi anamtumia mhusika Chuma kuukejeli uongozi na kusema kwamba “hata ambaye ni Mtemi ana baraka za mizimu”, kwani mambo wanayoyatenda pamoja na watumishi wao ni kinyume na ahadi walizotoa wakati wanachaguliwa kuiongoza jamii. Mwandishi anaonesha kuwa uongozi uliopo baada ya uhuru na wakati wa Ukoloni ni kama kubadilishana mabwana. Hii ni kejeli kwa viongozi wanaotawala kwa kutumia mbinu za Wakoloni walioondolewa nchini kwa wananchi kujitoa mhanga. Hata tunapoangalia ukurasa wa kumi na moja, mwandishi anatumia wimbo wa kejeli katika kudhihirisha hayo. Anamwonesha *Chiku* akiimba:

Wako wapi wanaojitapa

Tumeshawatimua, Hawapo tena

Matata na Ibenge wanamshangaa Chiku kwani wimbo huu hauna maana kwa kuwa mabwana bado wapo, kilichofanyika ni kubadilishana mabwana weupe kwa weusi ambao ni viongozi tulionao sasa.

Mwandishi huweza kutumia mbinu ya kicheko kama kejeli ili kuonesha wazi hali iliyopo katika jamii. Tunaona ukurasa wa thelathini na moja, anaonesha vijana waleta mapinduzi wanavyoangua kicheko dhidi ya viongozi. Mwandishi anaonesha jinsi tabaka la chini lina- vyofanya kazi kwa ajili ya kulisha viongozi na watumishi wao. Kwa mfano, Matata anaposema kwamba:

Mtemi na wenzake wanakula na kusaza.

Hata mbwa wao wanavimbiwa na kutoa ushuzi ovyo (...)

Hapa mwandishi anatuambia kuwa, Baada ya uhuru wananchi walifikiri wameondokana na udhalimu, utumwa, ufisadi, unyanyaswaji, unyonywaji na dhuluma kadha wa kadha. Wali- amini kwamba, viongozi waliowachagua na kuwaweka madarakani walikuwa tofauti kabisa na Wakoloni walioondolewa madarakani. Aidha, walikuwa wala rushwa, mafisadi, wazandiki na wenye kujichukulia madaraka mikononi. Wengi wao walipenda fedha kupita kiasi hivyo kudiriki hata kuwa na vyanzo vingi vya kujiingizia kipato. Hali hii ilipelekea kuanzishwa kwa kampeni na maazimio mbalimbali ya uboreshaji wa shughuli za serikali likiwemo Azimio la Arusha.

Ndipo walipomua kuanzisha Azimio la Arusha, kwa malengo ya kujenga ujamaa na kuji- tegemea. Kwenye sera ya Azimio hilo lililoanzishwa jijini Arusha, wananchi walihimizwa ku- fanya kazi kwa bidii ili na kuweza kujitegemea na kujiletea maendeleo wao wenyewe.

Katika kuhakikisha kuwa mipango yote na malengo yahasuyo sera hiyo yanafanikiwa, pakawekwa hadharani mashairi ya *Matunda ya Azimio* (mashairi ya mwamko wa siasa). Mambo kadha wa kadha yamejadiliwa kama vile Ujamaa na usawa, Uongozi, Uchumi, Ustawi wa jamii na Ulinzi na usalama na kudhihirisha *upekee* wa mashairi ya mwamko wa siasa. Mashairi haya yanajadili maudhui mbalimbali yakihusianisha na mfumo wa kisiasa uliokuwepo (Ujamaa).

KEJELI NA FASIHI YA KISWAHILI – TANZANIA

Honero na wenzake (1980) wanaukejeli umoja na ushirikiano kwa mashairi yao yasemayo: *Ujamaa ni Sadaka, Ujamaa ni Imani, Siasa ya Ujamaa na Umma na Unyonge Wetu*. Kwa mfano katika shairi la *Unyonge Wetu* ubeti wa pili linasema:

Ikiwatutaungana, unyonge tutaepuka
Iwapo tutaonyana, na maovu kuyasuka
Mabaya yatatukana, tutaishi tukicheka
Unyonge tutautoka, ikiwa tutaungana

Katika mashairi hayo, waandishi walikejeli nguvu watakayokuwa nayo baada ya kuungana kuwa ni sadaka, imani unyonge na mengine mengi kuukejeli utawala uliokuwa madarakani.

Kejeli ilitumika katika kipindi hicho ili kuonesha duara la maisha ya jamii na kuweka wazi utekelezaji wa sera zilizopangwa pamoja na malengo ya jamii. Mbinu hii ya kisanaa ilitumiwa na waandishi mbalimbali wa fasihi kwa kuzingatia uwezo wa kibunifu katika kuzingatia fani na maudhui ili kuwafikishia wahusika ujumbe murua. Kipindi hiki kilishuhudia kuanzishwa kwa vijiji vingi vya ujamaa kwa malengo ya kuwahimiza watu kufanya kazi kwa pamoja, kwa juhudi na maarifa ili kupata mali nyingi na kuzigawana kwa usawa.

Ngahyoma (1975) katika *Kijiji Chetu* anaweka wazi mambo yanayotendeka katika vijiji hivi. Katika kuifikishia jamii kile alichokusudia mwandishi ametumia kejeli katika kuonesha maendeleo ya ujamaa vijijini. Kwa mfano, *Ujamaa Mpya ni wa Kwenye Kitabu*. Maneno yalikuwa kejeli kwa viongozi wenye vyeo mbalimbali waliokuwa madarakani. Mwandishi anatushahisisha kwamba viongozi wetu tuliokuwa nao ni wa maneno bila matendo. Hivyo wana tangaza tu sera ya Ujamaa huku wao wanaenda kinyume na Ujamaa wenyewe.

Mwanafasihi huyu katika kazi yake hii ametumia *sauti* kama mbinu ya kisanaa ambayo inakejeli maisha ya jamii katika kuondokana na uongozi mbaya. Aidha mwandishi anaonesha kwamba wapo baadhi ya wanajamii wanaowasaliti wenzao katika harakati za kuleta mapi nduzi. Mwandishi kwa kutumia kejeli anaitaka jamii ifikiri, itafakari na kugundua mfumo huo wa maisha waliokuwa nao. Kwa mfano, ukurasa wa thelathini na saba, tunakutana na sentensi ifuatayo:

Sasa ulitaka maisha ya kikabaila au kibepari

Hapa mwandishi anawasha moto kwa jamii ili iweze kugundua kwamba hakuna haki wala usawa miongoni mwa wanajamii katika mfumo huu wa kijamaa.

Katika tamthilia ya Kezilahabi (1999) katika *Kaptula la Marx*, mwandishi amefanikiwa kutumia kejeli kama mbinu ya kuikosoa jamii na kusawiri mfumo wa maisha ya jamii ya Kitanzania. Jina la tamthilia *Kaptula la Marx* ni kejeli kwa mfumo mzima wa uongozi wa nchi za kijamaa. Mwandishi anafichua matendo yanayofanyika katika jamii yetu inayosadikiwa kufuata mfumo wa ujamaa na kujitegemea.

STEVEN E. MRIKARIA

Katika ukurasa wa kumi na saba, mwandishi anaonesha kukosekana kwa haki kulivyo-kithiri katika jamii husika. Mfano, amemwonesha mfungwa namba 3 anavyohukumiwa kifungo cha kwenda jela siku moja kwa kuiba mamilioni ya pesa za shirika la ndege, na akamwonyesha mfungwa namba 2 anafungwa miaka kumi na viboko ishirini na tano kwa kosa la kuiba mkate kwenye duka la Mhindi. Mwandishi ametumia mbinu ya *kicheko* katika kuukejeli mfumo mzima wa uongozi katika jamii hiyo. Mwandishi anaihamasisha jamii aliyoiita ya wakulima na wafanyakazi kuungana ili kuondokana na unyonywaji, unyanyaswaji na ukosefu wa haki. Katika ukurasa wa ishirini na nane, mwandishi ametumia sauti ya kejeli kuonesha kwamba mapambano hayo yapo na iwapo wataungana na kushirikiana, haki itapatikana. Ametumia maneno *Kipofu Anayeona Ni Hatari* kama kejeli kwa serikali ambayo haina msimamo kwa jamii yake.

Katika riwaya ya Ruhumbika *Miradi Bubu ya Wazalendo*, tunaona kuwa, ametumia jina la kitabu katika kukejeli jamii ya Kitanzania miaka ya sabini. Mwaka wa 1967 Tanzania ilishe-rehekea kuanzishwa kwa Azimio la Arusha la kujenga ujamaa na usawa. Ruhumbika anaeleza kuwa wananchi wote walitakiwa kuitana *ndugu* kwani mojawapo ya sera za Azimio la Arusha ilikuwa ni *Binadamu Wote ni Sawa*. Habari hizi zinaonekana katika riwaya hii ukurasa wa sitini na moja, ikisema:

Nchi nzima watu wote walikuwa wakiitana ndugu, waziri alikuwa ni ndugu waziri. Hata Rais ndugu rais, na waziri alimwita Said Ndugu (Mesenja Said).

Hata hivyo undugu huu haukudumu bali ulibaki mikononi mwa wachache tu. Kwa hakika neno *ndugu* ni kejeli kwa Azimio la Arusha, kwani hakuna undugu kati ya mtawala na mtawaliwa, masikini na tajiri, mwajiri na mwajiriwa, n.k..

Msanii mwingine aliyejitokeza katika uwanja huu wa kejeli ni Penina katika tamthilia yake ya *Lina Ubani* (1984). Mwandishi huyu anaonesha hali halisi ya ujamaa uliopo katika jamii yetu. Katika ukurasa wa thelathini na mbili, mwandishi ameandika:

Unasoma ujamaa? Acha mjukuu wangu akili yako itaharibika. Angalia baba yako kasoma sana ujamaa anasaidiana na mkewe kuninyima chakula.....Acha kusoma ujamaa....

Mfano huo wa bibi anapomwambia mjukuu wake asisome juu ya ujamaa ataharibu akili. Hii ni kejeli kwa mafanikio ya ujamaa kwamba hakuna yaliyo mazuri yanayoletwa na huo mfumo wa ujamaa. Hii ni kwa sababu sera ya ujamaa ilikuwa ya kuishi pamoja, kufanya kazi kwa pamoja na kwa manufaa ya wote.

Tunaonyeshwa pia kuwa kipindi cha miaka ya mwanzoni mwa 1980, kilikuwa ni kipindi kigumu sana kwa nchi na wananchi wa Tanzania. Kulizuka vita vya Kagera vilivyosababisha kupoteza maisha kwa Watanzania na hali yao ya maisha kuwa ngumu sana. Fasihi ya Kiswahili nayo katika kipindi hiki ilifichua na kuweka wazi matatizo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa yaliyokuwa yamekithiri nchini.

KEJELI NA FASIHI YA KISWAHILI – TANZANIA

Katika tamthiliya hiyo, Penina (1984) ametumia mbinu ya kejeli katika kusawiri vurugu, migogoro na mikanganyiko inayodhihirisha wazi kwamba bado kuna uvundo katika jamii. Jina la kitabu *Lina Ubani* ni kinyume na methali isemayo *La Kuvunda Halina Ubani*. Kejeli katika tamthilia hii imebeba ujumbe wa kazi ya mwandishi kwa kuonesha uozo uliokuwa umekithiri kwa viongozi ambao wana ubani. Hapa mwandishi ametumia mbinu ya *sauti* kuonesha uovu, fitina na ulaghai uliokuwa ukifanywa na viongozi. Haya ameyaonyesha ukurasa wa arubaini, aliposema kwamba:

Balaa limetukuta ndugu nawaambia Vita vya Dyamini havijesha tambueni.
(...) Lakini tunasema uzi uleule! Tutafunga mikanda. Tuyakabili yote...

Amesema hivyo akionyesha kuwa, jamii inahimizwa kuungana na kushirikiana ili kuleta mabadiliko.

Kwa kutumia mbinu ya majibizano kati ya mtambaji na mlevi, mwandishi ametumia *kilima* kama kejeli kwa viongozi. Kwa mfano, ametumia kilima cha Magharibi, mashariki, kati na Kaskazini. Dhana hii inaonesha chuki waliyonayo wananchi kutokana na mambo yanayofanywa na viongozi. Hii imeonekana dhahiri katika ukurasa wa arubaini na tano hadi ule wa arubaini na sita, mwandishi anadhihirisha haya pale Mwanahego anaposema:

Asiyefanya kazi wewe uliye juu ya kilima. Juu ya kilima kuna mashamba?
(...) kama kuzalisha mali ni kusema, kwa maneno yako tungeunda ndege. Basi niache Mwanahego niseme...

Tamthilia hii inatuonesha jinsi hali ngumu ya uchumi inayopelekea kupanda kwa bei za bidhaa na kwa baadhi ya mazao ya wakulima kukosa soko, hata inafikia hatua ya wakulima kung'oa mazao yao ya biashara. Penina (1984) anaonyesha viongozi wanavyohimiza kuzalishwa kwa mazao hayo ili waweze kufaidi wao wenyewe. Ameonesha jinsi ambavyo wakulima wasivyofaidi vema faida itokanayo na mazao hayo. Mwishoni tunaoneshwa jinsi wakulima wanavyoonekana kukata tamaa, katika ukurasa wa arubaini na sita:

Tunasikia kuna watu hawataki kulima Wanang'oa kahawa, wanang'oa chai, Taifa linategemea mazao hayo kupatia fedha za kigeni...

Maneno hayo yanasemwa na kiongozi, kwa kutumia mhusika Sauti. Mwandishi amemtumia Mlevi Mwanahego katika kukejeli mambo yanayofanywa na viongozi na kuonesha wazi jamii inakokwenda na ilikotoka.

Katika kipindi hiki cha miaka themanini, Tanzania ilikumbwa na janga kubwa la njaa. Hali ya maisha kwa tabaka la chini ilikuwa ya kutisha. Hali hii ya kutisha ilitokana na tamaa ya viongozi kujilimbikizia mali na kuhujumu njia kuu za uchumi. Maisha katika kipindi hiki yalifanana na yale ya kipindi cha Ukoloni, na hata pengine kuzidi ya kipindi cha Ukoloni. Katika kipindi hiki, fasihi ya Kiswahili ilisawiri jamii husika kulingana na matukio na mabadiliko yaliyojitokeza.

STEVEN E. MRIKARIA

Anatumia nafasi hii kuwakejeli viongozi waliokuwa wakijilimbikizia mali zao kwa wizi, uporaji na unyang'anyi na huku wakiwakamata wanajamii kama wezi, mafisadi na wahujumu wa uchumi. Ametutumia kejeli kuonesha kwamba sio wote waliokuwa wazuri kwa wakati huo.

Mvungi (1995) katika *Mashairi ya Chekacheka*, ametumia kejeli katika kuonyesha yale yaliojitokeza katika kipindi hiki hadi miaka ya tisini ambapo kulianzishwa mfumo wa vyama vingi. Mvungi ametumia jina la kitabu *Chekacheka* na baadhi ya vichwa vya mashairi yake katika kukejeli hali halisi ilivyokuwa katika jamii. Hivyo basi mbinu hii imemwezesha kwa kiasi kikubwa katika kugusa hisia za wasomaji na kufikisha ujumbe kuhusu masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kwa mfano, katika shairi la *Utu Umekua Kima* ukurasa wa kumi na nane, mwandishi anafichua wazi matendo ya viongozi walio katika tabaka la juu wanavyotumia mabavu yao katika kudhulumu na kuwanyonya tabaka la chini.

Mvungi amewakejeli wale viongozi wa vyama mbalimbali ambao hujifanya wenye kuwagiza walio chini yao kwa kuwalipa ujira mdogo huku waking'ang'ania wakidhani ndiyo hekima. Tabaka la chini hapa linachekelewa kwa kukejeliwa kuwa hata wakisemwa namna gani wasiache kutumika. Waendeleo tu.

Wakati mwingine, Mvungi amekuwa akionesha wazi maisha yalivyorudi nyuma kwenye kipindi cha utumwa. Kwa mfano, katika shairi la *Utumwa Uhuru* ukurasa wa ishirini na mbili, anaonesha kukosekana kwa demokrasia baada ya uhuru kupatikana. Bado viongozi wameshikilia enzi za Ukoloni, kichwa cha shairi hili ni kejeli juu ya uhuru na uongozi wa nchi za Kiafrika. Katika ubeti wa tatu tunasoma haya:

Pili ni utumwa huru, Afrika ilobaki
Matabaka yanadhuru, raia hawana haki
Ni maisha kwa ushuru, maisha ya shakishaki
Maisha yenye utupu, watu roho mikononi

Mwandishi anaonesha kukosekana kwa haki na demokrasia inayotokana na utawala wa chama kimoja. Katika shairi hili mwandishi anakejeli siasa ya nchi ambayo chama kimoja kinatawala. Hali hii hairuhusu demokrasia kwa wananchi kwani kila lilemwalo huwa ni sawa tu bila maamuzi ya wengi.

Vilevile katika shairi la *Gunia la Mikutano* ukurasa wa ishirini na tano, mwandishi anakejeli uongozi uliokithiri kwa unyonyaji, ulaghai, unyanyasaji na rushwa. Viongozi wamekuwa watu wa maneno tu na ziara ambazo huhitaji michango kutoka kwa wananchi. Ametumia neno *gunia* kukejeli mikutano na ziara nyingi wanazofanya viongozi huku wananchi wakiambulia patupu. Haya yanadhihirishwa katika ubeti wa tatu:

KEJELI NA FASIHI YA KISWAHILI – TANZANIA

Gunia la mikutano, pipa la maandamano
Hotuba kwa mashindano, kazi kubwa ni maneno
Michezo na michuano, haya ya mshikamano
Matokeo ni mateso, na kutojali shida.

Hali kadhalika katika kufichua mfumo mzima wa uongozi mbaya katika jamii mwandishi Mvungi ametumia kejeli kwa vichwa vya baadhi ya mashairi yake. Kwa mfano, shairi la *Chanzo cha Huo Uozo* ukurasa wa ishirini na nne, *Ulanguzi Umevaa Suti* urasa wa kumi na tano; na *Mtoto Aso Riziki* urasa wa ishirini na sita, n.k. Katika mashairi hayo mwandishi anaonesha rushwa iliyokithiri katika jamii ulaghai wa kisiasa, urasimu na matumizi mabaya ya mali ya umma. Hivyo basi mwandishi Mvungi katika diwani zake za *Mashairi ya Chekacheka* (1995), *Raha Karaha* (1978), na *Chungu Tamu* (1985) ametumia kejeli katika kufichua uozo uliopo katika jamii. Mwandishi ametumia mbinu hii kuonesha hali ya maisha, demokrasia, utabaka na uongozi mbaya. Hivyo basi mbinu hii imemuwezesha kwa kiasi kikubwa kufanikiwa kwa kazi zake kifani na kimaudhui.

Pamoja na fasihi ya Kiswahili kutumia kejeli kusawiri kwa kiasi kikubwa mfumo wa kiu-chumi na kisiasa kwa kuzingatia mabadiliko na matukio mbalimbali katika jamii; kejeli katika jamii hutumika katika kusawiri duara la maisha ya binadamu kwa kuwa kuna kupanda na kushuka na pia huwa na mwanzo na mwisho.

Kezilahabi (1988) katika *Karibu Ndani* ametumia dhana ya *chai* kuonesha mzunguko wa maisha ya binadamu kwamba ni duara hivyo hatuna budi kufanya yaliyo ya mafanikio wakati wa maisha yetu kwani mwisho wa maisha upo.

Katika shairi la *Chai ya Jioni* ukurasa wa tatu, ubeti wa kwanza tunasoma:

Wakati tunywapo chai hapa upenuni
Na kuwatazama watoto wetu
Wakicheza bembea kwa furaha
Tujue kamba ya bembea yetu
Imeshalika na imeanza kuoza
Na bado kidogo tutaporomoka

Katika shairi hili mwandishi amezungumzia maisha ya viongozi walioko madarakani. Anaonesha wazi jinsi viongozi wanavyofaidi wakiwa madarakani lakini pindi wang'atukapo hurudi katika hali ya kawaida. Hivyo anawakejeli kwa *chai ya jioni* akiwakumbusha kuwa wasijisahau kuwa ipo siku watayarudia maisha yaliyo sawa na ya wanajamii wengine. Haya yanadhihirishwa katika ubeti wa mwisho wa shairi:

Lakini kabla hatujaondoka kimyakimya
kukamilika nusu duara iliyobakia
tuhakikishe vyombo vyetu ni safi

STEVEN E. MRIKARIA

Hapa tunaona kwamba, pamoja na mwandishi kutumia kejeli katika kuonesha mfumo mzima wa maisha na uongozi, mwandishi ametumia pia mbinu hii katika kuonesha mabadiliko na mgogoro wa ushairi uliotokea miaka ya sabini.

Katika shairi la *Karibu Ndani* ukurasa wa thelathini na nne hadi ule wa thelathini na saba, mwandishi anazidi kukejeli mgogoro wa ushairi wa kimapokeo. Shairi hili la *Karibu Ndani* ni mwendelezo wa shairi la *Fungueni Mlango* lililo katika diwani ya *Kichomi*. Katika mashairi haya yote msomaji anakaribishwa ndani ajionee ushairi wa kisasa.

Katika sehemu ya kwanza ya shairi la *Karibu Ndani* mwandishi anaukejeli ushairi wa kimapokeo kwa kuufananisha na kibanda kikuukuu ambacho kinakaribia kuanguka, akimaanisha kuwa ushairi mapokeo hauna nafasi wakati huu, kwani muda si mrefu utakuwa ume-kwishapoteza watunzi pamoja na wasomaji wake.

Washairi wa mapokeo, sasa wacheza lala salama
katika mionzi hafifu, ya jua machweoni

Tunaona jinsi mwandishi anavyowakejeli wale walioshikilia mashairi ya kimapokeo waingie. Anawashauri katika mashairi ya kisasa yasiojali urari wa vina na mizani bali kuzingatia zaidi fani na maudhui. Hivyo basi mwandishi anahimiza washairi hao waende na wakati na kuacha mapokeo ushairi yaliyoigwa kutoka Ulaya na kufuata yale ya Kiafrika. Haya yapo katika ubeti huu wa pili:

Muda si mrefu patakuwa kiza tororo.
Kwenye kiza cha karne pasipo vichocho mkato
nilikuwa na nanga yangu, nyimbo mpya natongoa

Mwisho ukurasa wa thelathini na moja, mwandishi ameukejeli ushairi huo kwa kuulinganisha na mbwa aliyezeeka na asiye na meno aitwaye Mavina:

Nje kulikuwa na mwanga, nao ndege wakiimba
Kulikuwa na njia katikati, wanyama kila upande
Walioinamisha vichwa, kati nilipopita
Nilipouacha msitu, nyuma nilitazama
Mbali nilimwona Mavina, akitangatanga msituni

Mwandishi anatuonyesha kupotea kwa Mavina ambapo hawezi kugundua wala kubahatisha njia ya kurudi alikotoka. Anaukejeli ushairi wa kimapokeo kwa kuuashiria kupotea kabisa kwa sababu hauna mashiko na umepwaya.

3.3. Kejeli wakati wa utandawazi

Karne ya ishirini na moja kwa hakika imeshuhudia kuingia kwa teknolojia mpya katika nyimbo za Kiswahili. Teknolojia hii ilijiimarisha kwa kiwango cha juu na kupata mashiko na mwelekeo wa utandawazi. Utandawazi si mfumo mpya katika ulimwengu wa sayansi ya habari na teknolojia mpya. Mfumo huu umekuwepo kwa karne nyingi japo kwa viwango tofauti kutoka karne moja hadi nyingine.

Kuingia kwa dhana ya utandawazi katika fasihi simulizi kumeleta maingiliano na mabadiliko mengi Kitaifa na hata Kimataifa katika tanzu zake nyingi. Kwa upande wa mashairi na nyimbo maingiliano haya yanaonekana dhahiri na kuleta mabadiliko makubwa katika jamii.

Vijana wengi hususan wale wa Afrika ya Mashariki walizitumia mashairi yao kuielezea jamii juu ya matatizo wanayopambana nayo kila siku. Matalani ukosefu wa ajira, umaskini waliokuwa nao, athari za ukosefu wa ajira kwa vijana, uongozi, polisi, mahakama, n.k..

Kutungwa, kuimbwa na kuonekana majukwaani kwa wasanii na mashairi haya kumewezesha vijana kuwa wabunifu, wajasiriamali na weledi wa kueleza kero zao na matatizo wanayopambana nayo katika maisha ya kila siku. Kwa mfano, mashairi ya msanii Lion katika wimbo *Umasikini Huu*:

Umaskini huu (x 3) Utaisha lini

Umaskini huu (x 3) Utaisha lini

Umasikini huu (x 3) Utaisha lini

Msanii analalamikia kwa masikitiko makubwa umasikini uliokithiri Tanzania bila ya kupata jibu ya kuwa mwisho wake ni lini. Kwa upande mwingine anaikujeli nchi za Tanzania pamoja na viongozi wake ambapo kila siku wanaulalamikia huku nchi ni inao utajiri mkubwa wa raslimali. Hii inatuonyesha wazi kuwa msanii anaona uchungu sana juu ya umasikini unaozikumba nchi zetu ilhali viongozi wake ni matajiri.

Msanii Jaffer Rhyme yaliyopo wimbo wake wa *Niko Bize* yaani nina shughuli nyingi, anasema:

(...) ndiyo pekee inayonifanya nipate ninachotaka

Umenipata (brother) kaka ofisini hatujaliwi

Ndio sababu hasa tunasafa, Kwenye muziki cash tunapata

Niko Bize naandika rhyme kila time nnayipata

Sio bize tu for nothing, Bize nageti something

Kwenye life time hivi sasa kazi ni kazi afisa

Ili mradi tu inalipa ukiifanya kiuhakika

STEVEN E. MRIKARIA

Ni mfano mwingine wa kejeli inayowasema viongozi wa siku hizi. Kiongozi kila siku anakuwa safarini bila kujali nchi yake na wananchi wa eneo lake wanaishi namna gani. Kila siku kiongozi anapoulizwa jambo fulani yeye anajibu kuwa hana nafasi kwa kuwa ana kazi nyingi (*Niko Bize*). Kuwa *bize* huko hakumsaidii yeye wala wananchi wake bali hutumika kama fimbo ya kukwepea majukumu yake.

Kwa upande mwingine, msanii Jaffer Rhyme anaongeza kwamba wapo viongozi wengine ambao wako bize kwelikweli. Hawa ni wale waliomeza au walikunywa damu ya bendera. Viongozi hawa ni wale wenye kuona uchungu kwa wananchi wake. Hawa ni wale wenye kujitoa mhangwa kwa ajili ya kuitetea jamii nzima bila kujali uwezo walionao wanajamii. Pia hawa ni wale viongozi wanaokosa muda wa kuzurura ovyo na kupata nafasi ya kuwasikiliza wananchi waliowachagua. Maudhui ya mashairi haya ndio msingi mkuu wenye kujengwa na utandawazi.

Kwa upande mwingine tunauona mashairi ya Mr Ebbo katika wimbo wa *Mi Mmasai Bwana*:

Mi Mmasai bwana nasema mi Mmasai,
Nadumisha mila zile wengine walishashindwa,
Mi Mmasai bwana nasema mi Mmasai.
Naruhusu kushangaa kwa wageni na wenyeji,
Mi Mmasai bwana nasema mi Mmasai.
Tamaduni asilia ilobaki Afirika...

Msanii anatamba kwa kulisifia kabila lake la Kimasai, mila na desturi za Kimasai zilizomzunguka na ambazo zinazomshangaza kila mtu. Anasema kuwa hata utandawazi utandawae namna gani yeye hawezi kuuacha utamaduni wake huo. Mmasai huyu kwa namna moja au nyingine anawasema wale wote wenye tabia ya kuukana utaiifa wao na kuufurahia utaiifa wa wengine kuwa hawatafaidika lolote. Aidha mashairi haya yanazisema nchi na makabila mengi kuwa yameshindwa kudumisha tamaduni zao na kuiga tamaduni za kigeni.

Mashairi ya wasanii wengi yamegubikwa na kasumba waliokuwa nayo wanajamii wengi ya kuwa Kiingereza ni lugha ya wasomi. Kwa kasumba hiyo wasanii wanachanganya na lugha za Kiingereza na Kiswahili/Kabila jingine kama mbinu za kuwapata wapenzi wengi na wasomi. Kwa mfano mashairi ya msanii Lady JayDee katika wimbo wake *What I need from you is understanding*:

Ninachotaka kutoka kwako maelewano
What I need from you is understanding
nakupenda, nakutaka nakuhitajiii
I love you, I need you ...
Nakupenda, Nakutaka ...

KEJELI NA FASIHI YA KISWAHILI – TANZANIA

Msanii huyu pamoja na wengine wamesahau kwamba lugha ni kitu cha kujivunia kwa sababu ndio kielelezo cha utamaduni wa taifa. Aidha utamaduni ndio msingi na roho ya taifa lolote. Nchi ambayo haina Utamaduni wake yenyewe ni sawa na mkusanyiko wa watu wasio na *roho* ya kuwawezesha kujiita taifa.

4. Hitimisho

Tumeona kwamba kejeli haitumiki tu katika kuukosoa uongozi katika jamii, ni mzaha wenye kuweza kuwasema, kuwasengenya, kuwakebehi wanajamii wote kwa lengo la kuwarekebisha, kuwaonya na kuwaelimisha ili waende sambamba na wanajamii wengine. Kejeli haitumiki kwa lengo la kuwakosoa viongozi na watu wa tabaka la chini tu, bali hutumika kuwakosoa hata wanazuoni wenye kwenda kinyume na taaluma.

Kejeli ni mojawapo ya mbinu ambazo hutumiwa na wasanii na waandishi katika muktadha wa kuelimisha, kukosoa na kuburudisha jamii. Aidha, kejeli hutumika kwa malengo ya kuyaweka wazi mambo yaliyopo katika jamii, kulingana na mabadiliko na matukio yaliyopo na yanayotokea.

Kejeli hutoa uhuru wa waandishi na wasanii. Kwa hakika hii ni njia ya pekee sana ambazo inawapa wanajamii nafasi ya kushiriki kwa katika kuwakosoa walioko madarakani na kufanya kazi yao kuwa nyepesi kueleweka.

Katika kipindi cha ukoloni, kipindi cha baada ya ukoloni na kipindi tulichonacho hivi sasa cha utandawazi, mbinu za kejeli zimekuwa zikibadilika badilika. Hii inawezekana kwamba ni kwa sababu kadri ya mfumo wa maisha na mbinu mbalimbali za kupambana na mabadiliko hayo ya maisha zinavyobadilika, ndivyo na mbinu za kejeli zinavyobadilika. Kwa mfano hivi asa vijana wamebuni michezo ya kuchekesha inayorushwa katika baadhi ya vituo vya televisheni vya Tanzania kama vile *Ze Komedi* iliyokuwa ikionyeshwa kwenye EATV chaneli 5, *The Original Komedi* inayoonyeshwa na TBC *Mizengwe* inayoonyeshwa kwenye kituo cha ITV; na baadhi ya vituo vya televisheni vya Kenya kama *Vitimbi au Vioja Mahakamani* vinavyoonyeshwa na kituo cha KBC wanaitumia kejeli kuusema uozo, ufisadi, unyama, udhalilishwaji, unyanyapaa na ukandamizwaji ulioshika kasi katika jamii. Aidha vikundi hivi hutumia kejeli kuwasema wafanyakazi, wala-rushwa na wanajamii vigeugeu walioko na wanaoziongoza nchi na jumuiya mbalimbali. Kufanya hivyo kunaisaidia jamii iliyoko mbali na miji mikuu kufahamu kinachotokea ndani na nje ya nchi yao.

Vikundi vya vichekesho na dhana yao ya kejeli husaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza uchovu wa wanajamii baada ya shughuli nyingi na nzito za mchana kutwa. Hii ina maana kwamba jamii inapokusanyika pamoja na kuburudishwa kwa kuviangalia vikundi hivi vya vichekesho, inapunguza uchovu kwa kucheka na kufurahi. Hii pia ni kwa sababu, maigizo yanayo manufaa kwani yanabeba ujumbe muhimu ambao kwa hali ya kawaida hauwezi kubebwa na sanaa nyingine. Kwa mfano, suala la UKIMWI ni vigumu kuliongelea kwa urahisi bila kuigiza au kwa kuonyesha picha. Kwa kupitia vichekesho vyenye kejeli wana-

STEVEN E. MRIKARIA

jamii hujikuta wakiwa na shughuli za kufanya baada ya kazi na kujiepusha na mambo mengi yenye kusababisha maambukizo na usambazaji wa Virusi vya UKIMWI.

Ifahamike wazi kwamba, kejeli katika fasihi ya Kiswahili na kumbo zake hubeba ujumbe mzima wa kazi ya msanii au mwandishi kisaikolojia, kifani na kimaudhui katika kujikamilisha kwake.

Kwa mfano, wanamuziki wetu wa kizazi kipya, wana taarabu, wacheza maigizo, wachekeshaji, wanakomedia, wanakomiki na vikundi vingine vingi vya kisanii. hutumia kejeli kuielimisha jamii juu ya janga la madawa ya kulevya. Wasanii wetu hawa wamefanikiwa kwa kuiangazia misugvano iliyopo katika serikali, jitihada za kuinua uchumi, maisha bora, n.k..

Hivyo ni wajibu wa wasanii, waandishi na wanazuoni wengine kuhakikisha kuwa wanaitumia mbinu hii na kuiendeleza ili kufichua uozo, ubadhirifu, ufisadi, ufidhuli uliopo, unaojitokeza na unaozidi kujikita katika jamii na taifa zima kwa ujumla.

5. MAREJELEO

- Balisidya, M. L. 1982. *Uchunguzi katika fasihi simulizivizingiti na mkabala*. Katika makala za semina za TUKI na makala mbalimbali. Dar es Salaam. TUKI.
- Gibbs, R. W. 1994. *The Poetics of Mind. Figurative thought, Language & Understanding*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Honero, L. N. na wenzake. 1980. *Matunda ya Azimio la Arusha, Mashairi ya Mwamko wa Siasa*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili: Dar es Salaam.
- Kezilahabi, E. 1988. *Karibu Ndani*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Kezilahabi, E. 1999. *Kaputula la Marx*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Khatibu, M. S. 1988. *Fungate ya uhuru*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mbatiah, M. 2001. *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Fotoform Ltd.
- Mbogo, E. 1981. *Morani*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mtesigwa, P. C. K. 1989. *Methali ni nini? Katika Mulika juzuu Na. 56* Dar es Salaam: TUKI.
- Mhando, P. 1984. *Lina Ubani*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mvungi, T. A. 1985. *Chungu Tamu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mvungi, T. A. 1978. *Raha Karaha*. Dar es Salaam: Continental Publishers.
- Mvungi, T. A. 1995. *Chekacheka*. Dar es Salaam: Continental Publishers.
- Mwakyembe, H. 1980. *Pepo ya Mabwege*. Dar es Salaam: Longman.
- Mulokozi, M. M. 1989. *Tanzu za fasihi simulizi*. Katika Mulika juzuu Na. 21 Dar es Salaam: TUKI.

KEJELI NA FASIHI YA KISWAHILI – TANZANIA

- Ngahyoma, N. 1975. *Kijiji Chetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Penina, M. M. 1984. *Lina Ubani*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Ruhumbika, G. 1995. *Miradi Bubu ya Wazalendo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Rutashobya, M. G. R. 1980. *Nuru Mpya*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Kandoro, S. 1971 *Mashairi ya Saadani*. Dar es Salaam: Mwananchi Publishing Ltd
- Shaaban, R. 1951. *Kusadikika*. Nairobi: Nelson & Sons.
- Shaaban, R. 1968. *Kufikirika*. Nairobi: OUP.
- Short, M. 1980. *Style in Fiction*. London: Longman
- Wales, Katie 2001. *A Dictionary of Stylistics*. Harlow: Personal Education.
- Wamitila, K. W. 2008. *Kanzi za Fasihi. Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*: Nairobi Vide Muwa Publishers Ltd.